Karibia Ufanyike Mkristo

na

Ellis Forsman

Karibia Ufanyike Mkristo

na

Ellis Forsman

Oktoba 6, 2011

Karibia Ufanyike Mkristo

(Ambao Siyo Uongofu)

Matendo 26: 19-29

Katika Matendo 26: 19-29 tuna takwimu ya kutoongoka. Inamaanisha nini "kukaribia" Mkristo? Inawezekana kwa mtu kuwa muumini katika Kristo na asiwe Mkristo?

Mtume Paulo alipokuwa akiongea na Mfalme Agripa, akasema katika msitari wa 27, "… *Najua ya kuwa wawaamini."* Mfalme akajibu katika msitari wa 28, *"…Kwa maneno machache wadhani kunifanya mimi niwe Mkristo."*

Je Agripa alikuwa muumini? Au je alikuwa Mkristo?

Je Mfalme Agripa alikuwa Muumini?

Paulo aliposema katika msitari wa 27, *"Mfalme Agripa, je wawaamini manabii?*", hakika alikuwa anasema, "Je unamwamini Yesu Kristo kama jinsi alivyotabiriwa na manabii?". Hakuna shaka juu ya hili! Katika msitari wa 22 hadi 24 ya kifungu hiki, Paulo anawaelezea manabii na Musa kama watangazaji wa mambo manne:

- Ya kuja kwa Kristo.
- Kifo chake msalabani.
- Ufufuo wake kutoka katika wafu.
- Na uthamani wa injili Yake ya wokovu.

Alafu kwa uwazi na kwa kuuliza hilo katika katika mustari wa 27, "…*je wawaamini manabii?"* Ingepaswa aseme, "Je unamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu? Je unaamini kuwa alizifia dhambi zako? Je unaamini katika ufufuo wake kutoka katika wafu?"

Hakuwezi kuwa na shaka juu ya jibu! Biblia inaandika hitimisho ya Paulo mwenyewe katika maneno haya, *"…Najua ya kuwa wawaamini."*

Kweli, Mfalme Agripa alikuwa muumini? Ndiyo! Je alikuwa Mkristo? Hapana! Hakuna shaka kwamba Mfalme Agripa alikuwa muumini. Kutoka katika uhimara wake wa kumkiri Yesu Kristo, kusulubishwa kwake na kufufuka kwake, kama ilivyo tabiriwa na *"Manabii na Musa",* Paulo alishawishika kwamba Mfalme Agripa alikuwa muumini.

Kiukweli, alipomuuliza Mfalme Agripa, *"…je wawaamini manabii?"* , dhahiri alikuwa na uhakika na jibu.

Alafu, kwa maandishi yaliyofuata ya kalamu, Luka anaandika uhakikisho wa jibu la Paulo mwenyewe, "…*Najua ya kuwa wawaamini."*

Imani na Utii

Kutoka katika ukweli huu wa kutokubadilika tunaona umuhimu wa imani ikijionyesha yenyewe katika matendo – katika kutii mapenzi ya Mungu.

Kuna nadharia, inayofundishwa na watu wengi wa kidini leo, kwamba mwanadamu hawezi kufanya chochote ili aokolewe – kwamba wokovu katika Kristo ni kwa imani pekee – kwamba unachotakiwa kukifanya ni kuamini katika Bwana – hapo hapo, wakati tu ukiamini, bila muendelezo wa tendo lolote la utii – wokovu wako unahakikishwa.

Lakini, rafiki yangu, ni jinsi gani yalivyo maangamizi ya ajabu yanayoenezwa na ulimwengu wa kidini!

Mfalme Agripa alijua nadharia ya wokovu haikuwa ya kweli. Mtume Paulo alijua kuwa hitimisho la aina hiyo haikuwa ya kweli. Alijua kuwa mfalme Agripa alikuwa muamini, na pia alijua kuwa hakuwa Mkristo.

Paulo alikuwa akijaribu kumshawishi mfalme ili afanyike Mkristo, kama jinsi alivyokuwa Mkristo. Paulo alielezea uongofu wake kwa Mfalme Agripa mapema katika kifungu hiki.

Hataivyo Luka (ambaye aliandika kitabu cha Matendo Ya Mitume) hatowi mlolongo wote wa kuongoka kwa Paulo katika kitabu hiki, mtu anaweza kuwa na uhakika kwamba Mtume Paulo hakuacha chochote inje kwa jinsi alivyofanyika Mkristo.

Katika msitari wa 25, Paulo anaweka wazi kwamba anazungumzia "…*maneno ya kweli na ya akili*." Luka anatoa maelezo ya kina kuhusiana na kuongoka kwa Paulo katika sura za 9 na 22 ya kitabu cha Matendo.

Kitu kimoja ambacho mtu hapaswi kusahau, Sauli (kama jinsi Paulo alivyokuwa akiitwa kabla ya kuongoka kwake) ili elezwa na Yesu kwamba angeambiwa alichopaswa kufanya ili aokolewe (Matendo 9:6). Yesu alimwambia Sauli aende kwa Anania na angeweza kuambiwa anachoweza kufanya ili aokolewe. Na hakuambiwa kuamini pekee.

Kama kuamini ndiyo ilikuwa kitu muhimu, Paulo tayari alikuwa ameshafanya hivyo wakati aliposimama mbele ya Kristo na kumkiri. Paulo aliambiwa na Anania katika Matendo 22:16, "*Basi sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, ukaoshwe dhambi zako,ukiliitia jina lake*."

Kama Paulo alihusisha swala la wongofu wake kwa Mfalme Agripa katika jitihada zake za kumshawishi mfalme ili awe Mkristo – na alifanya kama jinsi tayari nimeshaonyesha – je hakusema "*ukweli"* kwa mfalme kuhusu wongofu wake kwa Kristo? Biblia inasema alifanya katika msitari wa 25.

Hivyo basi, je hakumjulisha mfalme kwamba yeye (Paulo) muamini aliyetubu ambaye alibatizwa katika Kristo ili kuoshwa dhambi zake, kama Anania mhubiri wa injili, alivyomuamuru? Yesu, Bwana wetu, alitoa mtiririko huo ili kwamba Paulo asiache hata moja.

Hapa kuna rekodi ya Luka kuhusu Paulo akiandika katika Matendo 22:3-16: Luka 22:3-16, "*Shetani akamwingia Yuda aitwaye Iskariote, naye ni mmoja wa wale Thenashara. Akaondoka akaenda akasema na wakuu wa makuhani na majemadari, jinsi atakavyoweza kumtia mikononi mwao. Wakafurahi wakapatana naye kumpa fedha. Akakubali, akatafuta nafasi ya kumsaliti kwao pasipokuwapo mkutano. Ikafika siku ya mikate isiyotiwa chachu, ambayo ilipasa kuchinja pasaka. Akawatuma Petro na Yohana,akisema, nendeni, mkatuandalie pasaka tupate kuila. Wakamwambia Wataka tuandae wapi? Akawaambia, tazama, mtakapoingia mjini mtakutana na mwanamume akichukua mtungi wa maji; mfuateni mkaingie katika nyumba atakayoingia yeye. Na mtamwambia mwenye nyumba, Mwalimu akuambia, Ki wapi chumba cha wageni, nipate kula pasaka humo pamoja na wanafunzi wangu? Naye atawaonyesha chumba kikubwa orofani, kimekwisha andikwa; andaeni humo. Wakaenda, wakaona kama alivyowaambia, wakaiandaa pasaka. Hata saa ilipofika aliketi chakulani, yeye na wale mitume pamoja naye. Akawaambia nimetamani sana kuila pasaka hii pamoja nanyi kabla ya kuteswa kwangu; kwa maana nawambia ya kwamba siili tena hata itakapotimizwa katika ufalme wa Mungu."*

Tunafahamu kwa hakika ni sehemu ipi uongofu wa Saulo iliyokuwa "kikwazo" kwa Mfalme Agripa. Tunaamini kuwa alikuwa muumini. Biblia inasema hivyo; Paulo alijuwa kwamba anaamini.

Tunajua kwamba Mfalme Agripa gakubatizwa katika Kristo ili kuoshwa dhambi zake, kama Paulo alivyofanya. Paulo akasema katika msitari wa 29 ya sura ya 26 ya Matendo, "…*Namwomba Mungu kwamba, ikiwa kwa machache au ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wote wanaonisikia leo wawe kama mimi isipokuwa vifungo hivi."*

Paulo alitaka mfalme kufuata mfano wake. Alimtaka mfalme afanye kitu ambacho alikuwa bado hajakifanya. Nani anaejua, labda amri ya Bwana ili kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi ili kuwa ni msitari wa utenganifu kati ya Mfalme Agripa kwa kufanyika Mkristo na si kuwa Mkristo. Hakika imekuwa ni hatua ya mwisho kwa mamilioni wengi wanaokataa kuwa Wakristo.

Mfanyakazi mwenzangu miaka kadhaa iliyopita aliniambia baada ya siku kadhaa ya majadiliano, “Najua Biblia inasema kwamba ni lazima ubatizwe ili uokoke, lakini nafikiri Bwana atafanya udhuru katika swala langu.

Ni katika misingi ipi ambayo mtu anaweza kutoa kauli kama hii?

Nasikia watu wengi wa dini wanasema kwamba kile tunacho kiitaji tu ni kumuamini Yesu, mpende Mungu, tuwapende binadamu wenzetu, alafu baadaye tutaokolewa; kwamba “upendo unatimiza sharia” (Waru. 13:10). Maandiko hayamaanishi kwamba upendo ndiyo mwisho wa sheria, lakini upendo wa kweli inamsababisha mtu kutimiza sharia yote.

- Math. 7:21, “*Si kila mtu aniambiaye Bwana Bwana ataingia katika ufalme wa mbinguni; bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.”* Hawa walikuwa ni waumini, lakini walikuwa hawafuati sharia ya Mungu.
- Luka 6:46, “*Kwa nini mnaniita Bwana, Bwana na hamfanyi yale niwaamuruyo?*” wanashindwa kuelewa kwamba “*upendo unatimiza sheria*” maandiko.

Lazima tusidharau dhumuni kuu la ukweli uliyofunuliwa na Mtume Yohana aliyevuviwa katika 1 Yohana 5:3, “*Kwa maana huku ndiko kumpenda Mungu, kwamba tuzishike amri zake; wala amri zake si nzito*.”

Rafiki zangu, mtu yeyote anaweza kusemaje kwamba kweli anampenda Bwana na kweli anamuamini, lakini anakataa kile anachokisema?

Itakuwa vizuri kukumbuka tabia ya Mafarisayo kuhusu Yohana Mbatizaji katika Luka 7:30, “*Lakini Mafarisayo na wanasheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye*.”

Mfalme Agripa, ambaye alikuwa “muamini”, alimkataa Bwana kama Mwokozi wake kwa kukataa kutii agizo la Bwana la kubatizwa – “kuoshwa” dhambi zake – kama Paulo alivyofanya.

Kulingana na tunavyojua, Mfalme Agripa aliyaacha maisha haya bila kujiandaa kumpokea Mfalme wa Wafalme Siku ya Hukumu itakapotimia.

Karibia uwe Mkristo siyo kwamba tayari umeshafanyika Mkristo!

Kuna nadharia inayofundishwa na viongozi wengi wa kidini kwamba hakuna kitu chochote ambacho mtu anaweza kufanya ili aokolewe. Hakuna anachoweza kufanya! Subiria tu uvuvio wa moja kwa moja wa Roho Mtakatifu, alafu moyo wake unatakasika, huwekwa mbali na dhambi, na anafanyika Mkristo.

Hakuna shaka, mmesikia watu wakiongea redioni, “Wewe weka mkono wako redioni; au, nyoosha mkono wako katikati ya watu; amini

tu kwa Bwana sasa; umkubali kama Mwokozi wako binafsi; hakuna la msingi; hakuna la ziada; sasa umeokolewa; sasa umeongoka kwa Kristo; sasa umekuwa Mkristo aliyezaliwa tena."

Rafiki zangu, msidanganyike! Huwezi kusoma kitu kama hicho katika Biblia maisha yako yote. Kimsingi haipo katika Biblia.

Mfalme Agripa hakuwa na udhuru, na unaweza ukawa na uhakika kwamba hakuna yeyote leo aliye na udhuru, vilevile.

Hata kama watu watakuwa wa kweli, tendo hilo na uamzi huo si wa uongofu – mtu ambaye hajaongoka ni sawa na swala la Mfalme Agripa.

Katika swala kama hili, nina shauku kwamba watu wengi "wanaongoka" kwa mhubiri, na si kwa Kristo.

Je tunapaswa kumshawishi Mungu au wanadamu?

Wanadamu wanatakiwa kushawishiwa ili wawe Wakristo kwa kuubiri injili. Wengi wanadhani yote wanayo weza kufanya ni kuamini alafu baadaye Roho Mtakatifu ataingia moyoni na kuisafisha. Je hiyo ndiyo Paulo alimfundisha Mfalme Agripa?, ambaye baadaye alijibu, "…*Karibia unishawishi ili niwe Mkristo*."

Nguvu ya ushawishi ilikuwa kupitia Paulo, mhubiri wa injili; si kwa Roho Mtakatifu moja kwa moja kutoka mbinguni. Paulo aliwatangazia Warumi katika Waru. 1:16, "*Kwa maana siionei haya Injili kwa sababu ni uweza wa Mungu uuletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza, na kwa Myunani pia.*"

Kuna wale wanaojaribu kumshawishi Mungu ili awakubali watu kama wanawe, wawe wamezaliwa mara ya pili au la kupitia utii wa neno la Bwana. "Eh, Mungu, waokoe wale wote walionyoosha mikono yao kwenye redio…"

Lakini Petro alijibu jinsi wanadamu wanavyozaliwa mara ya pili katika 1Petro 1:22-23: 1Petro 1:22-23, "*Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikilia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo. Kwa kuwa mmezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo, bali kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele*."

Hawa ni watu waliosikia, wakatubu, na walibatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao, kama ilivyofunuliwa katika Matendo 2:38, 1Pet. 1:1, na Matendo 2:9-11.

Tena, Ninawakumbusha, kwamba Mfalme Agripa alisema nguvu inayoshawishi moyo wake ilikuja kupitia ujumbe wa Paulo (msitari wa 27), si kwa kuingia moja kwa moja kwa Roho Mtakatifu.

Ndiyo, kuna wahubiri wanaomsii Mungu, kumuomba Mungu, “Waokoe watu hawa wanaokusubiria!” Lakini, rafiki zangu, hamjasoma kitu chochote kama hicho katika Biblia.

Je Mfalme Agripa alikuwa ni Mkristo? Hapana, hakuwa Mkristo.

Karibia kuwa Mkristo si kwamba tayari umefanyika Mkristo. Paulo alikuwa ni muumini na Mkristo vile vile. Mfalme Agripa alikuwa ni muumini na **siyo** Mkristo.

Hakuwezi kuwa na shaka kwamba Paulo alikuwa ni Mkristo. Na Biblia haiweki shaka kwamba Mfalme Agripa **Hakuwa** Mkristo. Mfalme mwenyewe alisema kuwa hakuwa Mkristo. “Karibia” ilikuwa ni kauli ya mfalme. Paulo alisema kuwa alijuwa kwamba Mfalme Agripa alikuwa muumini. Pia, alitambua kuwa hakuwa Mkristo.

Rafiki mpendwa, mtu hawezi kuwa Mkristo asipoamini, lakini si kila muumini ni Mkristo.

Je Paulo alikuwa ni Mkristo?

Mtume Paulo alijaribu kumshawishi ili awe Mkristo, kama jinsi yeye (Paulo) alivyokuwa Mkristo. Alihitimisha katika Matendo 26:29, “*Namwomba Mungu kwamba ikiwa kwa machache ama ikiwa kwa mengi, si wewe tu ila na hao wanaonisikia leo wawe kama mimi, isipokuwa vifungo hivi.*”

Swali kwa Paulo: “Wewe ukoje?” jibu linatolewa kwa njia ambayo si ya makosa, kwa msisitizo na uwazi, alisema, “*Mimi ni Mkristo*!”

Kumbuka, kama Mkristo, Paulo alitazamwa kutokuvaa na kuheshimu jina lingine isipokuwa jina la Kristo. Mtume aliwaonya waumini juu ya kanisa la Korintho kuhusu majina ya mgawanyiko na makundi; majina ya kidhehebu. Msikilize Mtume Paulo katika 1Wakor. 1:12-13, “*Basi maana yangu ni hii, ya kwamba kila mtu wa kwenu kusema, Mimi ni wa Paulo, na, mimi ni wa Apolo, na, Mimi ni wa Kefa, na, Mimi ni wa Kristo. Je! Kristo amegawanyika? Je! Paulo alisulubishwa kwa ajili yenu? Au, je! Mlibatizwa kwa jina la Paulo?*

Hitimisho kutoka katika kauli iliyovuviwa ya mitume inajulikana. Kristo, siyo Apolo, alisulubiwa kwa ajili yenu; mlibatizwa katika jina la Kristo, na si kwa jina la Paulo; Kristo hajagawanyika. Kwa hiyo, mnatakiwa kuvaa na kuheshimu jina la Kristo pekee.

Paulo alikuwa Mtume; alikuwa ni mtu mkuu wa Mungu, lakini hakuna mtu anayepaswa kuvaa jina lake.

Petro alikuwa Mtume; Yule ambaye Bwana alimpa funguo za ufalme (Math. 16: 18-19), ambayo ilitumika siku ya Pentekoste (Matendo 2, wakati hotuba ya kwanza ya injili ilipohubiriwa na Petro. Nafsi 3000 zilibatizwa katika Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi.) Bado, ingekuwa ni makosa kulitii jina la Petro.

Hitimisho la Mungu la moja kwa moja kupitia Paulo ilikuwa: Kristo alisulubiwa kwa ajili yenu; kwa iyo, vaa jina la Kristo pekee.

Watu husema, "Ni kitu gani ambalo lipo katika jina? Jina si muhimu!"

Paulo alionyesha kwamba jina lilikuwa ni muhimu kwa sababu Kristo alilifia kanisa. Alitoa damu yake kulinunua kanisa. Matendo 20: 28, "*Jitunzeni nafsi zenu na lile kundi lote nalo, ambalo Roho Mtakatifu amewaweka kuwa waangalizi, ili mpate kulilisha kanisa la Mungu, ambalo amelinunua kwa damu yake mwenyewe*."

Petro alieleza katika Matendo 4:10-12, "*Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye ninyi mlimsulubisha, na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina hilo mtu huyu anasimama ali mzima mbele yenu. Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo*."

Ninyi mliobatizwa mlibatizwa katika jina la Kristo; kwa iyo, vaa jina la Kristo, na siyo iyo ya Petro, Paulo, Apolo, Lutha, au mtu mwingine awaye yote, au mfumo, au mafundisho, au kitengo cha wanadamu, bali jina la Kristo Pekee.

Kristo hajagawanyika; hivyo, vaa tu jina Lake.

Paulo alikuwa Mkristo. Alijaribu kumshawishi Mfalme Agripa ili afanyike Mkristo, lakini alishindwa. Mfalme Agripa akasema, "…*Karibia unishawishi ili niwe Mkristo*." Karibia ni kushindwa; karibia ni kupotea!

Ni maneno gani haya yenye uvuvio wenye maana yanayotoka katika 1 Petro 4:16, "*Lakini ikiwa kwa sababu ni Mkristo asione haya, bali amtukuze Mungu kwa jina hilo*."

Wakati wa Agano Jipya, wale ambao kiukweli wali ongoka kwa Bwana waliitwa Wakristo. Matendo 11:26, "*Hata alipokwisha kumwona akamleta Antiokia. Ikawa kwa muda wa mwaka mzima wakakusanyika pamoja na kanisa na kuwafundisha watu wengi. Na wanafunzi waliitwa Wakristo kwanza hapo Antiokia*."

Je wewe ni Mkristo? Au je unakaribia kuwa Mkristo?

Jinsi gani mtu anavyofanyika Mkristo? Zifuatazo ni hatua muhimu za kufanya hilo liwezekane:

- **Imani.** Waeb. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza yeye: kwa maana yeye amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wote wamtafutao*." Nilipokuwa katika kidato cha tano (nilikuwa na umri wa miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wa kwangu akaniambia kwamba haamini kwamba Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimesha batizwa, Nilichukua muda wa kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kwamba anaweza kuona kwamba kuishi maisha ya Ukristo ilikuwa ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba kuna Mungu. Lakini ilikuwa awe upande salama, labda anapaswa kwenda kanisani, na atakapokufa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna siku ya hukumu), labda kama Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na kuishi maisha mazuri kwamba Mungu atamuruhusu kwenda mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "Haiwi hivyo. Lazima umwamini kwa moyo wako wote la sivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Matendo 2:38, Matendo 2: 38, "*Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu*." Matendo 11:18, "*… Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletalo uzima*." Kama ulikuwa unalala, ukasikia kelele kwenye chumba kingine, na unafikiria mwenyewe, "Kuna mwizi katika nyumba hii!" Taratibu unachukua simu ya mkononi, na kuwapigia polisi, ukiwaambia kwamba kuna mwizi ndani ya nyumba yako, na unawapa namba ya nyumba. Muda mfupi, wanafika na kumkamata mwizi. Anapiga kelele, na kusema, "Samahani; Samahani!" Anaomba msamaha wa nini? Kwa sababu amekamatwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi ageomba msamaha kwamba hataiba na kwamba anataka kubadili maisha yake ili kwamba asiibe tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Ni badiliko la nia linalopelekea badiliko la tendo. Hicho ndio tunatakiwa kufanya kabla hatuja fanyika Wakristo.

- **Kukiri.** Waru. 10:9-10, "*Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu*." Tunakiri nini? Kwamba tunaamini kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu kwamba imani (kuamini), kutubu, na kukiri ni "**KATIKA**" haki, uzima au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu fulani; si kwamba mtu ameshapata.

- **Ubatizo.** Ni katika ubatizo ambapo haki, uzima, na wokovu zinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kutimiza haki yote, uzima, na wokovu vinapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kutimiza haki yote, "*Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye*." (Math. 3: 14-17). Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni kitu sahihi kukifanya. Umeona jinsi ilivyompendeza Mungu wakati Yesu alikuwa akibatizwa? Yesu pia alisema "*imekuwa kwetu* ***sisi*** *kutimiza haki yote*." Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki Yake, siyo kwa sababu ya haki yetu.

  Kwa hakika, tusipo batizwa, bado tungali katika dhambi zetu. "*Petro akawambia, Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi zenu, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matendo 2:38). Petro, umesema sababu ya ubatizo ni nini? "*Kwa ajili ya ondoleo la dhambi*". Kwa nini mtu aache hatua hii muhimu inayoondoa dhambi zetu?

  Yesu aliagiza kwamba ili kuufikia wokovu ni lazima tubatizwe. "*Akawambia, Enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa*." (Marko 16: 15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu hiki hiki, "*Sasa unakawilia nini? Simama, ubatizwe, na uoshwe dhambi zako, ukiliitia jina la Bwana*." (Matendo 22:16).

  Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake: kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima*." (Waru. 6:4). Utu wetu wa kale lazima ufe. "*Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti Yake: Kusudi kama Kristo*

alivyofufuka katika wafu kwa injia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena." (Waru. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu kwa kutumia damu ya Yesu katika maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru na dhambi zetu za zamani pale tu tunapo batizwa.

Hii haimaanishi "kunyunyiza. Andiko hilo hapo juu linasema ubatizo ni maziko. Hatupeleki mwili makaburini na kuuwekea udongo kidogo; tunauzika.

Kama haujafanyika Mkristo, kwa nini usizingatie leo?